لا اله الا الله محمد رسول الله

ان الدّين عندالله الاسلام

## MTUME MUHAMMAD S.A.W. NI

# MFANO MWEMA

## KWA WATU WOTE

ISBN 9987 - 438 - 03 - 2

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

# UTANGULIZI

*Makala hii imeandikwa kutokana na ile makala ya Kiurdu iliyoandikwa na marehemu Hazrat Mir Muhammad Ishaque, mwanachuoni mkubwa wa mambo ya dini (Mungu awe radhi naye) na shemeji wa Seyidna Ahmad A.S. na imetafsiriwa kwa Kiswahili na Bwana B. K. Heri.*

**Baada ya kupata UHURU, wenyeji wa Afrika wamepata madaraka makubwa ya kujichagulia wenyewe vitu vya kuwafaa na kuvitupilia mbali baadhi ya vile vilivyowachukiza. Sio katika uwanja wa siasa, elimu na biashara tu Waafrika wamepanuka maoni, bali upande wa dini vile vile wamekuwa na busara zaidi na tangu sasa watakuwa na madaraka ya kujichukulia mafunzo yenye faida nyingi kwao maishani, hapa duniani na huko akhera.**

**Uamuzi utakaofanywa sasa utakuwa na athari kubwa – mbaya sana ikiwa umeamua vibaya na nzuri mno ikiwa umeamua vizuri wala – hutapata mwingine kwa kumlaumu. Zamani Mwafrika akishika njia ya upotovu alitaka kujiponesha kwa kusema ya kuwa ameshurutishwa kuishika ile. Lakini baada ya kupatikana UHURU mwovu hatapata nafasi ya kumlaumu mwenzie eti amempoteza, bali kujilaumu nafsi yake.**

**Basi wakati huu ni wa hadhari mno. Na baada ya kuwatanabahisha ndugu zote Waafrika tunaweka mbele yao kwa ufupi maisha ya MTU MKAMILIFU yule ambaye alikuwa mwanadamu kama sisi, lakini kwa sababu ya utukufu wa mwendo wake na usafi na unyofu wa moyo wake alipaa juu sana–juu kuliko wanadamu wote.**

**Ndugu msomaji, ukiwa wewe ni Mwislamu tafadhali fikiri, je unafuata katika nyayo za mtu huyu ambaye ni MFANO MWEMA kwa ajili yako; na ikiwa ni Mkristo, tafadhali fikiri kwa makini sana kama waweza kumchukua MWANADAMU HUYU MKAMILIFU KWA KILA UPANDE awe Kiongozi wako katika maisha yako; na ukiwa hujaanza kusoma dini yo yote katika hizi mbili, tafadhali uzichungue sana habari zifuatazo ili upate kumfanya MPENZI HUYU WA MWISHO WA MWENYEZI MUNGU awe ndiye mwalimu wako na mlezi wako katika mambo yote. HUU NDIO WAKATI WA KUAMUA.**

**Sheikh Muhammad Munawwar**
**Mbashiri wa Islam**

**Salaam Mosque,**
**Sultan Street, Dar-es-Salaam.**
**12 Rabi-ul-Awwal, 1381 Hijriyyah Qamariyyah.**
**24 Zahur, 1340, Hijriyyah Shamsiyyah.**
**24th August, 1961.**

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ

Mtu anajifunza kwa kutazama mfano. Nguo tunayovaa, lugha tunayosema, na hasa maisha tunayoishi, yanakuwa maigano kwa upande mmoja au mwingine. Mtu angekuwa haigi, hangelikuwa jinsi alivyo leo.

Watu wa mataifa mbali mbali walipokuwa wakiishi mbali mbali, kila taifa liliishi kwa namna yake. Lakini siku hizi watu wa mataifa mbali mbali wanaishi pamoja, wanataka njia moja ya kuwaongoza wote pamoja.

Na nani anaweza kuwaongoza wote sawa? Ni yule aliye mkamilifu katika kila kitu. Kama angelikuwa mpungufu katika kitu cho chote, wafuasi wake wangelipotea. Kwa hiyo ni mtu aliye mkamilifu kwa kila hatua ya maisha, ndiye anastahili kufuatwa na watu wote. Ni mtu asiye na doa, kwani vinginevyo kutakuwa hakuna imani kubwa kwake. Ni mtu ambaye historia ya maisha yake ni sifa nzuri tupu na matendo mazuri, ili kuwa mfano mzuri wa kufuata.

**Mtu Mkamilifu:**

Tunafurahi kusema kwamba upelelezi wetu umefaulu kugundua mtu ambaye ni mkamilifu katika kila mwendo wa maisha. Huyu mtu ni Muhammad (amani na baraka za Mungu ziwe juu yake).

Mwenyezi Mungu anasema katika Kurani Tukufu:
“Bila shaka mnao mfano mwema katika Mtume wa Mwenyezi Mungu” (33:22).

Na kwa kuwa ni lazima mtu aliye mfano kwa wengine asiwe na makosa, akasema wazi wazi:

“Hakika nimekwisha kaa kati yenu umri mwingi kabla ya hayo, je, hamfahamu” (10:17).

Kwa maneno hayo Mtume alisema sawa sawa kabisa.
Nani anaweza kumpata na doa katika maisha yake? Hakika hangeweza kudanganyika haada ya kupata utume.

Na kwa kuwa kutokuwa na doa tu, hakutoshi kwa yule anayeigwa, Mwenyezi Mungu kasema:
“Na bila shaka (Ewe Muhammad) una tabia njema, tukufu” (68:5).

Madai ya mtu kuwa mfano yanatakiwa yawe na ushahidi wa dalili kabla ya kukubaliwa. Wakristu wakimchukua Yesu kuwa mfano mzuri, Mabaniani wanawafikiria Marishii wanne kuwa mfano mzuri. Kwa hiyo lazima tuwe na njia hasa ya kushika kwa kufikia uamuzi.

Ni dhahiri kuwa ni yeye tu anaweza kuwa mfano mzuri, akiwa amekutana na hali zote za maisha wanazokutana nazo watu wengine. Vinginevyo ingelikuwa kwamba katika mambo ambayo hakuyapata, hangeweza kuwa mfano. Kwa hiyo hebu tutazame mahali na hali za maisha ya watu mbali mbali na matatizo yanayowatatiza maishani kisha tuchungue ni nani kati ya watakatifu na Mitume hao anayeweza kufanywa awe mfano kwa sababu ya kupitia hali hizo zote. Na hii hapa ni orodha yetu ya mambo makubwa hasa katika maisha ya wanadamu ambayo kwayo atakiwa kiongozi na mfano:

1. Mfano mwema kwa mayatima.
2. Mfano mwema kwa watoto.
3. Mfano mwema kwa vijana.
4. Mfano mwema kwa wazee.
5. Mfano mwema kwa kapera.
6. Mfano mwema kwa mwenye ndoa.
7. Mfano mwema kwa mzazi.

8. Mfano mwema kwa ndugu.
9. Mfano mwema kwa rafiki.
10. Mfano mwema kwa jiranl. ..
11. Mfano mwema kwa maskini.
12. Mfano mwema kwa kibarua au mtumishi.
13. Mfano mwema kwa tajiri.
14. Mfano mwema kwa mwenye kuajiri wengine.
15. Mfano mwema kwa bwana.
16. Mfano mwema kwa raja.
17. Mfano mwelpa kwa watawala.
18. Mfano mwema kwa wafalme.
19. Mfano mwem;a kwa maaskari katika hali! ya kushinda na kushindwa.
20. Mfano mwema wakati wa dhiki.
21. Mfano mwema wakati wa hali kubadilika kuwa nzuri.

Hizi ni hali mbali mbali za maisha ambazo mtu huweza kukutana nazo. Na hakika yatakuwa ni majisifu tu ikiwa mtume fulani atatajwa kuwa mfano mzuri na hali yeye hakupitia katika hali zote hizi, au kusema jinsi alivyozipitia.

Hebu sasa tuwatazame mitume wote wa zamani. Tuanzie mitume wanne waliotajwa na Vedas (kitabu kitakatifu cha Baniani). Jambo wanaloweza kusema wafuasi wao ni kuwa hao (mitume wanne) walikuja miaka bilioni na bilioni iliyopita, na kuwa wao hawakuwa na baba wala mama. Hatuna habari kama walioa au hapana, na kama walizaa watoto au hawakuwa na watoto. Na wala hatuna habari kama walipata kupigana vita au hapana.

Kwa kweli hatuna habari nao kama vile mifano yetu hapo juu inavyoonyesha. Sasa wanawezaje kuwa mfano mzuri?

Tuje sasa kwa Yesu Kristu. Habari za maisha yake yote hatujui. Tunajua sehemu ndogo sana. Yeye tunaambiwa alikuwa maskini

maisha yake yote, kwa hiyo hawezi kuwa mfano mwema kwa matajiri. Siku zote alikuwa raia, kwa hiyo mfalme hawezi kupata mfano mwema wo wote wa mambo ya kutawala kutoka kwake yeye (Yesu Kristu). Hakupata kupigana kwa hiyo washindi wa vita au wanaoshindwa hawawezi kupata kwake cho chote cha kuwaongoza katika mambo ya vita na amani. Yeye hakupata kuoa bibi, kwa hiyo anaweza kuwa mfano mwema kwa wale tu wasiotaka kuoa. Lakini wale ambao wanaoa, hawasaidiwi naye. Hatuwezi kumwona katika maisha yake akifundisha jinsi ya kutunza mke nyumbani, watoto, na namna ya kuwatuliza wafiwa. Mzee akifiwa na watoto wake, Yesu at amwambia kuvumilia tu. Lakini yule mzee akimwuliza je! bwana na wewe ulipata kupatwa uchungu kama huu nimepata mimi? Yesu atasema “Hakika mimi sikupata machungu ya kufiwa na watoto. Maisha yangu yote sikupata kuoa”.

Ni dhahiri kuwa kitulizo gani mzee huyu maskini atatazamia kupata kwa maneno matupu haya?

Isitoshe, Yesu hakufanya kazi kwa mtu ye yote au kufanya biashara yo yote. Anawezaje basi kuwa mfano mwema kwa mfanya biashara, tajiri au mtumishi. Alikuwa mtu aliyejiweka katika hali ya umaskini. Na anaweza tu kuwa mfano mwema kwa wale wanaojiwekea nadhiri ya umaskini.

Yeye akakamatwa na adui zake, akatiwa jela na kusulubiwa msalabani. Basi anaweza kuwa mfano mwema kwa wale watu wanaokutana na mikosi ya namna hiyo. Katika maisha yake yote, walakini, hakupata kuwashinda adui zake hata tuweze kujifunza kwake jinsi alivyopambana na adui hao na jinsi alivyowashinda na alivyowatendea!

Tena, Yesu hawezi kuwa mfano mwema kwa mzee, kwa sababu kwa kufuata Injili yeye hakufikia uzee. Na wala hawezi kuwa mfano mwema kwa mgonjwa, kwa sababu habari zake zote juu ya maisha

tunayosoma, hatuoni kama alipata kuugua. Hakuwa na jirani, mjane, au yatima chini ya mamlaka yake. Kwa hiyo hawezi kuwa mfano mwema kwa wote hawa.

Kwa mambo ya hali kama hizi, Yesu hawezi kuwa mfano mwema kwa jinsi orodha yetu iliyo juu inavyoonyesha. Tunaweza kusema tu kuwa yeye ni kweli alitumwa kwa wana wa Israeli. Lakini kwa wakati huu dunia imekuwa pana au tuseme watu wa mataifa mbali mbali wamekuwa karibu karibu, Yesu hawezi kuwa mfano mwema kwa dunia nzima hii.

Hebu sasa tuje kwa Muhammad (amani na baraka za Mungu ziwe juu yake). Hakuna hata mfano mmoja katika mifano yetu hiyo juu, ambao hauhusiani naye katika maisha yake. Namna ya maisha yake ni ya kushangaza sana kwa jinsi yalivyojaa matendo mema na mafanikio. Na cha kushangaza zaidi ni kuwa maisha mafupi yake ya Madina alikoishi miaka kumi tu, matendo yake yote yakahifadhiwa. Mtu gani anaweza kusadiki kuwa maskini, yatima huyu angeweza kuandika yote haya? Inakuwa kama vile hadithi za kubuni. Lakini sifa ya jinsi maisha yake yalivyoandikwa, hata maadui wa Uislamu wanakubali kuwa ni sifa nzuri ya pekee.

Hapa tunaandika kwa ufupi jinsi maisha yake yanavyokuwa mfano mwema kwetu.

### Mfano Mwema kwa Yatima

Baadhi ya watoto hufiwa na baba zao wakiwa bado wachanga, na baadhi ya watoto hufiwa na baba zao wanapokuwa watoto wakubwa kidogo. Lakini Mtume Muhammad s.a.w. alizaliwa yatima. Baba yake alifariki miezi mitatu kabla yake (Mtume) kuzaliwa. Mama yake akafariki dunia. Mtume akiwa na umri wa miaka sita. Na hata hivyo huyu yatima wa mayatima alikuwa na adabu njema na mpole hivi hata akawa kipenzi sana wa babu yake na ndugu na jirani wote wakampenda. Hii ilikuwa kwa mpango kuwa akue mwenye tabia nzuri sana.

Hebu mayatima wachukue mfano mwema kwa Mtume s.a.w. Wawe na adabu njema, tabia nzuri na miendo ya upole nao wataweza kuwapendeza watu wanaokuwa karibu nao. Amani iwe juu ya Muhammad, yatima!

### Mfano Mwema kwa Watoto, Kijana na Mzee

Lakini sio mayatima peke yao. Watoto wote kwa jumla wafuate mfano wake (Mtume s.a.w.). Yeye akalelewa na babu na mjomba wake ambao walikuwa badala ya wazazi wake. Hebu watoto washike mfano wake wa jinsi alivyokuwa mpole, mwenye adabu, mtii, na msaidizi wa kazi za nyumbani. Wataona kuwa wazazi wao wanawapenda sana na nyumba zao zitawapendeza.

Mtume s.a.w. alikuwa mfano mwema katika maisha yake yote. Alipokuwa mtoto hakuwa anazurura-zurura hovyo. Alipokuwa kijana alijilinda kukaa vema bila ya kwenda huko na huko. Na alipofikia uzee, hakuwa mwenye kuchoka na kukaa kivivu.

### Mfano Mwema kwa Kapera

Hali ya joto katika Bara Arabu inawafanya watu wafikie ujana upesi sana. Lakini hata hivyo, Mtume s.a.w. alikaa kapera mpaka alipotimiza miaka ishirini na tano. Na akaishi maisha matakatifu sana yasiyo na ila. Acha mbali urafiki wo wote na mwanamke, hata hakufikiria kumtazama. Amani iwe juu ya Muhammad, kapera!

### Mfano Mwema kwa Mwenye Ndoa

Ingawa Mtume s.a.w. alikuwa na wake zaidi ya mmoja, isipokuwa mke mmoja tu, wengine wote walikuwa wamefiwa na waume zao au wamepewa talaka. Na wote hawa akawatendea wema na kuwatunza kwa upole na mapenzi makubwa hata kusema: “Mbora

katika ninyi ni yule anayemtunza mkewe vizuri, nami nawatunza wake zangu vizuri zaidi”.

Acha kusema kuwa hakupata tu kuwapiga wakeze, hata kuwaambia maneno makali hakupata kuthubutu.

Bibi Khadija (radhi ya Mungu iwe kwake) alikuwa na umri wa miaka arobaini, alipoolewa na Mtume s.a.w. akiwa na miaka ishirini na tano. Wakakaa kwa muda wa miaka 15 wawili mpaka alipofariki dunia Bibi Khadija. Mtume s.a.w. akamwoa mke wa pili Bibi Aisha (radhi ya Mungu iwe juu yake) akiwa kigori bado. Naye anasema:-
“Sijapata kamwe kumwonea sivu mwanamke ye yote ila Bibi Khadija ambaye alikufa miaka mitatu kabla sijaolewa na sikumwona. Sababu ya kumwonea wivu ni kuwa kila mara nikamsikia Mtume akimsifu sana”.

Mtume s.a.w. alikuwa akikumbuka sana Bibi Khadija (radhi ya Mungu iwe juu yake) hata kila alipochinja mbuzi au kondoo, akawa anawapelekea sehemu ya nyama shoga zake.

Bibi Aisha anasema:-
“Wakati mwingine Mtume alikuwa akinikuta nikicheza na shoga zangu, nao walipomwona anaingia wakakimbia. Lakini yeye aliwarudisha na kutuambia tuendelee tu kucheza”.

Mtume s.a.w. akazoea kuwachukua naye katika safari zake. Na katika kazi zao za nyumbani alikuwa akiwasaidia.

Kwa desturi ya Mayahudi na Mabaniani, mwanamke anapokuwa mwezini, anafikiriwa kuwa mchafu kwa hiyo haruhusiwi kuingia jikoni, chumba cha kulia chakula, na hata kulala kitanda kimoja na mumewe. Lakini Mtume s.a.w. akaondoa desturi hii. Wakeze walipokuwa katika hali hii, yeye alikula nao, kulala kitanda kimoja nao, na hata kusoma Kurani akiwaegemea.

Kabla ya kufika kwa Mtume s.a.w. wanawake katika Bara Arabu walikuwa hawawezi kuwarithi waume zao. Ni yeye aliyewapa haki hii ya kurithi.

Hata karibu kwake kufa alionyesha huruma sana kwa wanawake hata kuwahimiza masahaba wake kuwatendea mema wake zao.

Alikuwa akiwaheshimu sana wakeze hivi hata siku moja alipoambiwa na mkewe kuwa asali anayopenda sana kunywa inamwachia harufu, siku ile ndio ilikuwa mwisho wake kunywa tena asali mpaka hapo alipoamrishwa na Mwenyezi Mungu asijinyime kilicho halali.

Wakeze nao wakampenda sana sana hata wakatamani kujua ni yupi ambaye atakuwa wa kwanza kukutana naye huko peponi baada ya kufa.

Huo ndio mfano mwema mtu anaweza kushika kwa kutendea wema mkewe.
Amani iwe juu ya Muhammad, mfano mwema kwa wenye ndoa!

## Mfano Mwema kwa Mzazi

Mtume s.a.w. alikuwa na watoto wengi. Kwa kuwalea aliangalia kukua kwa miili yao, tabia na roho zao. Akakuza tabia ya kujiheshimu kwa watoto wake. Na moja ya maneno yake ni “waheshimuni watoto wenu”.

Ilikuwa kwa sababu ya mafundisho yake tu ndio binti yake mpenzi Fatuma alipata daraja ya kuitwa “Bibi wa Peponi”.

Vifo vya watoto huwa ni misiba mikubwa sana kwa rnzazi. Naye Mtume s.a.w. akafiwa na watoto wake wote wa kiume na binti zake karibu wote ila mmoja tu alipokuwa hai. Hata hivyo akavumilia

machungu yote, na uvumilivu wake ni mfano mzuri pamoja na maneno yake haya:-

“Kile kinachochukuliwa ni Chake Yeye. Na hata kile anachotoa ni Chake Yeye”.

Na wakati wa kilio alikuwa akijituliza kwa maneno haya ya Mwenyezi Mungu: “Hakika sisi tu wa Mungu na Kwake tutarejea” (Kurani 2:157).

Mwanae Ibrahim alipokaribia kufa, akiwa amemwegemea baba yake (Mtume s.a.w.) yeye Mtume s.a.w. alikuwa akitokwa na machozi. Abdul Rahmani bin Auf, mmoja wa masahaba wake wakubwa akafikiri kuwa hili ni jambo la ajabu. Lakini Mtume s.a.w. akasema: “Ewe bin Auf, mapenzi na huruma hii, machozi yanatiririka na moyo unajaa machungu; lakini hatusemi lo lote ila Iile linalompendeza Yeye. Hakika sisi tu wa Mungu na Kwake tutarejea”.

Amani iwe kwake Muhammad, mfano mwema kwa mzazi!

**Mfano Mwema kwa Ndugu**

Mtume s.a.w. alikuwa akiwatendea mema ndugu zake hata wale ambao hawakukubali Uislamu. Naye anasema hivi:-

“Hakika wale ambao hawakukubali Uislamu sio ndugu zangu kwa Imani. Lakini ni jamaa zangu na kwa hiyo nawapa haki yao”.

**Mfano Mwema kwa Rafiki**

Hakupata kuwapa nafasi rafiki zake kunung’unika, kila mara akawa mwema kwao. Makka iliposhindwa, watu wa Ansar walihuzunika wakifikiri kuwa sasa atawaacha na kuhamia Makka. Yeye

akaondoa huzuni kwa kuwaahidi kuwa yeye ataendelea tu kukaa Madina. Na katika wasia wake aliagiza kwa Khalifa wake kuwaangalia watu wa Ansar.

**Mfano Mwema kwa Jirani**
Alikuwa jirani mzuri sana. Alikuwa akiwaomba wakeze kuongeza mchuzi ili jirani zake nao wapate. Na alipokaribisha watu kwenye chakula, alifikiria kwanza jirani zake.

**Mfano Mwema kwa Maskini na Watumishi.**

Kwa kawaida watu wa Mashariki hawajui heshima ya kazi. Kazi nyingine wanazidharau, hawawezi kuzifanya hata wanakuwa tayari kufa kwa njaa kuliko kufanya kazi za namna hiyo. Yeye Mtume s.a.w. alizaliwa katika nyumba ya watu mashuhuri kabisa katika Makka. Hata hivyo hakusita kufanya kazi za mikono. Na anasema:- "Chakula kizuri zaidi ni kile kinachopatikana kwa jasho la mkono".

Alipokuwa kijana akachunga mbuzi wa watu wa Makka kwa mshahara mdogo. Alipokua zaidi alikubali kuajiriwa na Bibi Khadija (radhi ya Mungu iwe juu yake) hata mwisho akawa msaidizi wake katika mambo ya biashara.

Hivi alipitia namna zote za kazi za maisha ya mfanyakazi hata kumpatia sifa ya kuwa mfano mwema kwa mfanya kazi.

Maskini huelekea kuomba-omba, kuwaonea uivu matajiri. Kudokoa pengine mali ya watu, pia pengine kukopa na hali wanajua kuwa hawawezi kulipa madeni yao. Lakini Mtume s.a.w. hakuwa hata na moja ya aibu hizi. Alipewa sifa ya "mwaminifu". Alipokopa alirudisha pamoja na faida kidogo. Alichukia kabisa kuomba-omba na akakuza tabia ya kujiheshimu kwa masahaba wake kuwaambia kuwa mmoja wenu akiangusha bakora ni vizuri zaidi kuiokota mwenyewe kuliko kumwomba mtu mwingine.

Huyu ndiye maskini Muhammad s.a.w. Ikiwa maskini wataiga mfano wake watashinda matatizo mengi na wataona kuwa umaskini wao sio kitu.

## Mfano Mwema kwa Tajiri

Hata huyo maskini Muhammad, amani na rehema kwake, alipokuwa tajiri sana, aliishi maisha mepesi tu. Hakutumia pesa zake kwa kununua vitu vya starehe za dunia. Aliwaambia wazi wazi wakeze:-

"Mkitaka maisha haya ya dunia na anasa zake, njooni nitawapeni na mkatoke kwangu kwa uzuri na salama". (28:29).

Alikuwa akiwapa wakeze pesa za kutumia kwa matumizi ya lazima tu na pesa zilizobaki akawapa maskini, watumwa waliopewa uhuru au akazitoa kwa matumizi ya nchi nzima.

Barabara za mjini zilijaa watumwa aliowanunua ili wapate uhuru wao. Alikuwa mkarimu hivi hata aliweza kumpa maskini mmoja ngamia mia moja. Namna alivyotumia pesa zake inaweza kuonekana kwa jinsi wazee wa Makka walivyokuwa wakimsema kuwa anatumia pesa zake kama vile haogopi kuwa anaweza kufilisika.

Katika wasia wake aliagiza kuwa mali itakayobaki baada ya kulipia gharama zote na kuwagawia nusu ya kawaida wakeze, igawanywe kwa maskini. Na yeye ndiye wa pekee katika watoa sheria ambaye alitoza kodi kubwa (Zaka) mali iliyolala bure bila kufanya kazi.

Ikiwa matajiri watafuata mfano wake, dunia haitakuwa na pazia, upande mmoja ukomunisti na upande mwingine utajiri wa kikundi kidogo cha wtu. Kwani utajiri ukiwa sio kwa kuwatumia maskini tu, maskini hawawezi kuwachukia matajiri.

## Mfano Mwema kwa Matajiri na Mabwana

Hazrat Anas anasimulia:-

“Nilianza kazi kwa Mtume s.a.w. nilipokuwa na umri wa miaka kumi tu. Nikaendelea kuwa mtumishi wake mpaka alipokufa. Na hakuna hata siku moja aliyonitukana au kunifyokea. Kama mtoto mdogo nilipotumwa nje, nilisahau pengine nilichotumwa nikacheza barabarani. Mtume s.a.w. akaja pengine nyuma yangu na kunikamata kichwa au sikio”.

Mkewe Bibi Aisha anasema:
Mungu ni shahidi wangu kuwa Mtume s.a:w. hakupata kumpiga mtumishi wake”.
Zaid, aliyekuwa mtumwa wa Bibi Khadija (radhi ya Mungu iwe kwake) naye akampa Mtume s.a.w. Siku moja kaka na baba yake Zaid walimwendea Mtume kumwomba ampe uhuru Zaid. Mtume akasema yeye (Zaid) yuko huru kwenda popote anapotaka. Lakini kwa kuwa Zaid alikaa vizuri sana na Mtume s.a.w., alikataa kwenda pamoja na baba na kaka yake na alimtanguliza Mtume juu yao. Amani iwe kwake Muhammad, tajiri na bwana.

## Mfano Mwema kwa Raia

Kama raia wa nchi, Muhammad (amani na baraka ya Mungu iwe kwake) alichukia sana kuleta uchochczi kwa serikali iliyowekwa. Mateso aliyokuwa akipata yeye mwenyewe na masahaba wake yalipozidi aliwaambia masahaba wake kukimbia Makka kwenda Habeshi na baadaye yeye mwenyewe alikimbilia Madina. Lakini hata hivyo alibakia mwaminifu kwa serikali ya Makka, hakupenda hata mara moja utumiaji wa nguvu. Baadhi ya masahaba zake walipomshauri kukamata silaha aliwajibu:-

“Hamkufundishwa kurudisha nyuma mkono wenu?”

Ikiwa raia wanafuata mfano wa Mtume s.a.w. ghasia na uasi mwingi unaozuia maendeleo havingetukia.

**Mfano Mwema kwa Wafalme na Watawala**

Akiwa mtawala wa Makka, Mtume s.a.w. hakukusanya mali kwa faida yake mwenyewe. Wala hakuwapendelea zaidi ndugu na jamaa zake.

Katika vita ya Badr askari hodari watatu wa Kikureshi walipojitolea kwa mapigano, aliwaamuru akina Ali, Hamza na Abu Ubaidah jamaa zake wa karibu kukutana nao. Na iliwezekana kabisa kama wangeweza kuuawa na mashujaa hao wa Makka. Angeweza kuwapeleka Makureshi wengine Waislamu waende kupambana nao, lakini alitaka kutoa mfano kwa kujitolea.

Alikuwa mwenye kupenda haki hivi hata sahaba mkubwa na rafiki yake sana, Athumani, alipotaka kumpendelea mhalifu, yeye Mtume s.a.w. alimwambia “Oh! Athumani unataka kuingilia sheria ya Mungu? Hakika ikiwa binti yangu mwenyewe, Fatuma, angeiba ningemkata mkono”.

Wafalme kwa kawaida huwa na mawazo kuwa watu wapo kuwatumikia wao. Lakini Mtume s.a.w. alisema: “Kiongozi wa taifa ni mtumishi”. Na mawazo haya ndiyo hasa yalivyokuwa sawa na maisha yake. Hakupenda kamwe watu wamsifu, wamfunge kilemba cha ukoka, wamsimamie kwa kumtukuza anapopita kama mfalme wao. Hata siku moja mtu mmoja alipotetemeka mbele yake, yeye (Mtume s.a.w.) alisema: “Mimi ni mwana wa mjane maskini tu ambaye kwa sababu ya umaskini ikampasa kula nyama kavu”.

Sio kama wafalme wengine, yeye aliishi maisha ya kawaida tu yasiyokuwa na anasa. Alifanya kazi zake zote sawa sawa kwa utaratibu kabisa. Alikuwa akisalisha sala tano kila siku, sala ya

Ijumaa, Idi, pamoja na kutoa hotuba, kuongoza sala za jeneza, kuwasomea adhana watoto mara tu wanapozaliwa, kuwatazama wagonjwa na kuwashauri dawa za kutumia, kutengeneza viatu vyake vikipasuka, kuwasaidia wakeze kazi za nyumbani, kufanya mazoezi ya kiaskari, kutuma askari, kuchagua maofisa, kupandisha bendera zao, kuwapa silaha na kutoa mashauri kwa askari, kusikiliza shida za watu, kukata mashauri, kutengeneza mipango kwa manufaa ya maskini na wale watumwa waliopewa uhuru, kutengeneza mikataba na kufanya kazi nyingine za kila siku. Hivi hakuna hata wakati mmoja alipata kukaa hivi hivi tu. Alipumzika wakati wa usiku tu. Hata hivyo kati kati ya usiku aliamka na kusali hata miguu yake ikavimba kwa kusimama kwa muda mrefu katika sala. Na alikuwa akisali kwa unyenyekevu hivi mbele ya Mwumba wake hata kulia machozi akisoma aya hii:-

“Oh! Bwana wangu ukiwaadhibu, wao ni viumbe Wako. Na ukiwasamehe, Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye hekima”.

Hakumweka askari au mchungaji ye yote mlangoni. Wanaume, wanawake na watoto waliweza kuingia nyumbani mwake kama kawaida bila ya kizuizi cho chote. Alikuwa akiwauliza Anas na Abu Huraira, (wa kwanza mtumishi wake na wa pili sahaba wake) kuwaita maskini waje wanywe maziwa wakale tende na tamu tamu. Kila jioni baada ya Sala ya Magharibi alichukua ndani ya msikiti kikundi kidogo cha maskini nyumbani mwake kula nacho chakula.

Hakupata kamwe kutumia mali ya serikali kama vile mali yake mwenyewe-: Siku moja akamkuna ngamia mgongoni akisema:-

“Siruhusiwi mimi kuchukua kitu kidogo kama nywele hizi na kukifanya mali yangu zaidi ya haki yangu ya desturi”.

Katika kazi za taifa alikuwa akifanya kazi kama mtu wa kawaida. Wakati wa kujenga msikiti wa Madina yeye pia alikuwa akichukua

mawe ya kujengea. Alipoona hivi mshairi mmoja miongoni mwa Ansar, alilia:-

“Tunakaa kitako Mtume akifanya kazi,
Fedheha gani hiyo na Ubaya gani huo!”

Katika vita ya Ahzab, alipokuwa akichimba handaki sahaba mmoja akamwendea akimwonyesha tumbo lake alilolifunga mkanda kwa kutuliza njaa. Mtume s.a.w. naye akamwonyesha lake, naye alikuwa amefunga kanda mbili kwa sababu hiyo hiyo.

Nchi ya Arabia iliyojaa wizi na uhalifu mwingi sana iligeuka mara Mtume s.a.w. alipoanza kutawala. Mwanamke akaweza kutembea peke yake bila ya hofu yo yote.

Maadui wake walimwogopa sana hivi kwamba mwenyewe Mtume s.a.w. alisema:-

“Nimetukuzwa sana hata maadui wananiogopa hadi masafa ya mwezi mzima”.

Huyu alikuwa Muhammad, Mfalme na Mtawala! Amani iwe kwake!

## Mfano Mwema kwa Shujaa

Ilikuwa kwa sababu ya amri yake ndio watoto, wanawake, wazee, walimu wa dini na waliojeruhiwa wasiumizwe au kuuawa wakati wa vita. Wanyama na miti pia isiharibiwe bure. Na kuwa hakuna hata maiti ya mtu aliyekufa vitani ilichomwa moto.

Katika vita ya Uhad kulikuwa maiti nyingi za Waislamu pamoja na ya Hamza, mjomba wake (Mtume s.a.w.) zilikuwa zimekatwa katwa mikono na miguu. Lakini yeye licha ya kuwa alikuwa amekasirishwa sana na vitendo hivyo, akasema itakuwa sio vizuri kwa Waislamu kukatakata maiti za maadui zao.

Katika vita ya Badr, Waislamu waliwateka watu sabini, naye Mtume s.a.w. akaamuru kuwa lazima watunzwe vizuri. Mateka hawa wanasimulia kwamba Waislamu waliweza kutembea kwa miguu nao (watumwa) wakipanda ngamia au farasi; Waislamu waliweza kukosa chakula au maji wakawapa mateka hawa.

Kwa kawaida wafalme na majemedari wanafuatana na maaskari kwa kuwapa moyo tu, waila wanajiweka pa salama sana. Lakini Mtume s.a.w. alikuwa tu katikati ya vita kama watu wengine. Hata mtu shujaa kama Ali anasema kwamba kwa kupumzika kidogo vitani walikuwa wakienda nyuma yake Mtume.

Tena inajulikana kwamba majemedari na maofisa wengine wa jeshi huwa wanakimbia vita inapokuwa mbaya upande wao. Hata inasemwa kuwa Napoleoni alifanya hivyo katika vita ya Waterloo. Katika vita ya Uhud, Waislamu walikuwa karibu wamezungukwa na maaaui, na katika vita ya Hunain, mwanzoni mwake, walizungukwa kabisa. Lakini hakupata kamwe Mtume s.a.w. kukimbia!

Katika vita ya Hunain jeshi lake liliposambaa yeye mwenyewe mtu mmoja alirudisha mashambulio ya maadui. Sahaba mmoja alipotaka kumkamata nyumbu wake, Mtume s.a.w. alitoa amri amwache na aliendelea mbele akisema:

“Mimi ni Mtume na sio uongo. Na mimi ni mwana wa Abdul Muttalib”.

Amani iwe kwake Muhammad, shujaa!

**Mfano Mwema kwa Wenye Dhiki**

Kwa muda wa miaka mitatu Mtume s.a.w. alizuiwa katika bonde la “Shebi-Abi-Talib”. Asiweze kupata msaada wo wote kutoka nje.

Nabii Yusuf A.S. aliweza kupata chakula gerezani. Lakini watu wa Makka hawakuruhusu kipande cha mkate kiende kwa watu waliokuwa katika bonde la Shebi-Abi-Talib. Hata kelele za watoto wadogo usiku kucha hazikuweza kulegeza roho ngumu za watu wa Makka. Lakini Mtume s.a.w. hakurudi nyuma hata chembe. Alishikilia ujumbe wake mpaka ususaji ukamalizika.

Amani iwe kwake Muhammad, mvumilivu!

**Mfano Mwema wakati wa Bahati**

Mwanzoni Mtume s.a.w. alikuwa amekataliwa na hajulikani. Baadaye akawa kiongozi wa taifa. Alipokimbilia Madina kutoka Makka aliondoka na sahaba mmoja tu – Abu Bakr. Lakini siku ya kurudi Makka aliingia na watu elfu kumi. Na hata hivyo hakubadili kamwe tabia yake. Wakati wa dhiki na umaskini alijiheshimu na wakati wa uwezo na sifa alikuwa mnyenyekevu na mtaratibu. Mafanikio hayakugeuza kichwa chake kama vile shida hazikubadili moyo wake.

**Mfano Mwema kwa Mshindi**

Kwa muda wa miaka 13 katika Makka na miaka minne Madina, Mtume s.a.w. alipata taabu sana kutokana na maadui zake. Alikuwa akipingwa yeye na masahaba wake. Wakiteswa na kutukanwa bure. Walikokotwa na ngamia, wakauawa na wake zao. Wakatupiwa takataka na mateso ya namna nyingi sana.

Kwa mateso ya namna ile mtu anaweza kufikiria kulipiza kisasi. Lakini haikuwa hivyo kwa Mtume s.a.w. alipoingia Makka pamoja na masahaba elfu kumi. Mtume s.a.w. alisahau kabisa maovu yote aliyotendewa yeye na masahaba wake, naye akasema:-

“Nendeni zenu ninyi wote mu huru. Hakuna cha kuwalaumu. Mungu awasamehe. Naye yeye ni mwingi wa Rehema kwa wale waonyeshao huruma”.

Nabii Yusufu A.S. aliwasamehe ndugu zake. Na kama hangewasamehe angelimwudhi sana baba yake. Na uhalifu au ukatili waliofanya kaka za Nabii Yusufu A. S. haukulingana hata na ubaya wa watu wa Makka. Wao kaka zake (Nabii Yusufu A. S.) hawakutaka ndugu yao afe. Walimtupa tu kisimani kwa matumaini kuwa wasafiri wakimwona watamtoa (12:11). Lakini watu wa Makka walikusudia hasa kumwua Mtume s.a.w. Tena kaka za Nabii Yusufu A. S. walimtupa kisimani. Lakini watu wa Makka waliendelea kumshambulia hata alipokimbilia Madina. Kwa hiyo huruma ya Nabii Yusufu A. S. kwa kaka zake hailingani na ya Mtume s.a.w. kwa watu wa Makka. Alimsamehe hata yule mwanamke ambaye alitafuna ini la mjomba wake. Alimsamehe yule mtumwa aliyemwua mjomba wake. Alimsamehe mtoto wa Abu Jahali, adui mkubwa.

Kwa huruma yote hii haiwezi kulingana na huruma yo yote katika historia. Amani iwe kwake Muhammad, Mshindi, Msamehevu. Huyu ndiye Muhammad, Mtukufu,
Mtume wa Mungu. Mfano mwema na Kiongozi wa viongozi wote.

***UMCHUKUE MTUME MUHAMMAD AWE KIONGOZI WAKO WA DAIMA!***